

**MTIHANI WA PAMOJA
MUHULA WA TATU 2023
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA KWANZA 102/1**

1. Hii ni insha ya kiuamilifu inafaa kuwa na sura na maudhui.

SURA.

Iwe na sehemu zifuatazo:

- ❖ Anwani- itaje kumbukumbu ni za nani.
- ❖ Wakati. Na mahali.
- ❖ Majina ya wahusika waliohudhuria.
- ❖ Majina ya waliokosa kuhudhuria.
- ❖ Kufunguliwa kwa Mkutano.
- ❖ Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu.
- ❖ Kujajidili mambo yanayotokana na kumbukumbu zilizopita.
- ❖ Nafasi ya kuandika sahihi ya mwenyekiti ziachwe wazi.

Hoja

- ❖ Upungufu wa vitabu vya Kiswahili.
- ❖ Idadi ndogo ya walimu wa Kiswahili.
- ❖ Matumizi ya sheng' shuleni.
- ❖ Athari ya lugha ya kwanza.
- ❖ Kutomaliza silabasi.
- ❖ Vipindi vichache vya Kiswahili katika ratiba ya shule.
- ❖ Mielekeo hasi kuhusu somo la Kiswahili.
- ❖ Sera duni kuhusu somo la Kiswahili.

2. Hii ni insha ya kujadili au kufafanua hoja.

Hoja ziweze kuzungumziwa madhara ya ufisadi na vilevile suluhu.

Baadhi ya hoja za madhara ni:

- ❖ Kutopata huduma muhimu bila hongo.
- ❖ Kusambaratika kwa uchumi wa taifa.
- ❖ Kutupiliwa mbali kwa mitihani ya kitaifa.
- ❖ Watu kufutwa kazi kwa sababu ya ufisadi.
- ❖ Kuharibu mazingira.
- ❖ Kufungwa jela kwa wahusika.
- ❖ Viongozi kupoteza nyadhifa zao.
- ❖ Kuleta fedheha kwa familia.

Baada ya hoja za suluhu:

- ❖ Kuhamasisha wananchi kuhusu athari za ufisadi.
- ❖ Kutia mbaroni wahusika na kuwashtaki.
- ❖ Kutaifisha mali iliyonyakuliw kwa njia ya ufisadi.

Tanbihi:

Mtahiniwa aweze kufafanua angaa hoja tano kikamilifu.

3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali hii

Ukicheza ujanani utalipa uzeeni.

MATUMIZI

Hutumiwa kuwahimiza watu wajitahidi kujitengenezea maisha yao ya kesho/mustakabali wao wakiwa wangali na uwezo wa kufanya hivyo.

TANBIHI

- ❖ Mtahiniwa sharti aandike kisa kitakachodhihirisha maana ya methali

- ❖ Kichwa kionyeshe pande mbili za methali:
 - kucheza ujanani
 - kulipa uzeeni
- ❖ Mtahiniwa atakayerejelea upande mmoja atakuwa amepungukiwa kimaudhui. Insha yake isizidi alama **10**
- ❖ Atakayeandika kisa kisichohusiana na methali hii atakuwa amepotoka kimaudhui. Atuzwe alama **03**.
- ❖ Atakayejitungia swali na kulijibu atuzwe **BK 01**
- ❖ Dhana ya kulipa uzeeni ijitokeze hata kama ni kwa aya chache/sentensi chache.

4. Hii ni insha ya mdokezo

Maneno kiini ni kutenda mema na kuwa umetendea nafsi yako. Mtahiniwa atunge kisa ambacho kitaoana na mdokezo. Mtahiniwa anaweza kutumia mbinu rejeshi ili kuonyesha wema mhusika aliutenda. Hatimaye aonyeshe vile mhusika huyu aliweza kutendewa wema kama alivyotenda.

Tanbihi:

Mtahiniwa atakuwa amepotoka pale tu kisa chake kitakuwa kimekosa kuoana na mdokezo.

Atakapokosa kumalizia na kidokezo atakuwa tu amepungukiwa kimtindo lakini hajapotoka.